

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

Anwani ya Simu: "TUME"

**DODOMA**

Nambari ya Simu: 0738 166 703

0733 005 974

Barua pepe: [secretary@psc.go.tz](mailto:secretary@psc.go.tz)

Tovuti: [www.psc.go.tz](http://www.psc.go.tz)



Tume ya Utumishi wa Umma,  
Jengo la Chimwaga (UDOM),  
Ghorofa ya Pili,  
2 Barabara ya UDOM,  
S.L.P. 1074,  
**40405 DODOMA.**

08 Machi , 2024

**Kumb. Na: LA.218/247/01/47**

## TAARIFA KWA UMMA

### UTANGULIZI

Tume ya Utumishi wa Umma (PSC) ni Idara Inayojitegemea chini ya Ofisi ya Rais iliyoundwa kwa Mujibu wa Kifungu cha 9 cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 (Marejeo ya Mwaka 2019).

Majukumu ya Tume ni pamoja na kutoa ushauri kuhusu masuala ya usimamizi wa Raslimaliwatu katika Utumishi wa Umma, kushughulikia Rufaa na Malalamiko ya watumishi wa Umma ambao hawajaridhika na uamuzi uliofanywa na Mamlaka zao za Ajira na Nidhamu na kufanya urekebu kwa kuhakikisha kuwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu zinatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia Utumishi wa Umma.

Kwa Mujibu wa Kifungu cha 25 cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 (Marejeo ya Mwaka 2019) kikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 60 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022, Mamlaka za Rufaa katika Utumishi wa Umma zimebainishwa kuwa:-

- (i) Tume ya Utumishi wa Umma (PSC), na
- (ii) Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, Kifungu cha 10(1) (d) na (g) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 (Marejeo ya Mwaka 2019) kimeipa Tume mamlaka ya kupokea na kushughulikia

Rufaa na Malalamiko ya Watumishi wa Umma mtawalia ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa na Mamlaka zao za Nidhamu na Ajira.

Tume katika kutekeleza jukumu hili, kuanzia tarehe 19 Februari, 2024 hadi 08 Machi, 2024 Jijini Dodoma, chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Jaji (Mst.) Hamisa Hamis Kalombola pamoja na Makamishna wa Tume, ilifanya Mkutano wake wa Tatu wa mwaka 2023/2024 kupitia Rufaa na Malalamiko yaliyowasilishwa mbele yake..

Katika Mkutano huo, jumla ya Rufaa na Malalamiko **342** yaliwasilishwa na kutolewa uamuzi katika mchanganuo ufuatao:-

- (i) Rufaa **160** zilisikilizwa na kutolewa uamuzi, na
- (ii) Malalamiko **182** yalisikilizwa na kutolewa uamuzi.

Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 62(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, Warufani **21** na Mrufaniwa mmoja (**01**) walitumia haki yao ya kisheria kufika mbele ya Tume na kutoa ufafanuzi wa hoja zao za rufaa na malalamiko.

Katika Mkutano huo wa Tatu wa Mwaka 2023/2024, makosa yaliyoonekana kutendwa zaidi ni pamoja na; utoro kazini, kuajiriwa bila kuwa na sifa, kukiuka Maadili ya Utumishi wa Umma, wizi, uzembe na kushindwa kutekeleza majukumu na kusababisha hasara kwa Mwajiri.

Wakati wa Mkutano huu, Taarifa mbalimbali za Utendaji wa Tume ziliwasilishwa na kujadiliwa, zikiwemo; Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya mwaka 2022/202, Taarifa ya Ukaguzi wa Uzingatiaji wa Sheria katika usimamizi wa Utumishi wa Umma ya mwaka 2023/2024, Taarifa ya Utendaji Kazi wa Tume ya Robo ya Pili ya mwaka 2023/2024 na Taarifa ya Utafiti kuhusu Utoro Kazini kwa watumishi wa Umma ya mwaka 2024..

Tume inaendelea kuwakumbusha Watumishi wa Umma kuzingatia Sheria ili kujiepusha na vitendo vinavyoashiria ukiukwaji wa maadili au uvunjifu wa sheria, hali inayoweza kusababisha Mamlaka zao za Nidhamu kuwachukulia hatua za nidhamu au kuwafikisha mahakamani kwa makosa ya jinai.

Vile vile, ni muhimu kwa Mamlaka za Nidhamu kutambua kuwa moja ya misingi ya kutoa haki ni kwa mtumishi mtuhumiwa kupewa fursa kujitetea kabla ya kuhukumiwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu na Sheria zilizopo. Ni wajibu wa mamlaka hizo

kuhakikisha hilo linazingatiwa ili haki si tu itendeke bali ionekane inatendeka kabla, wakati na baada ya usikilizwaji wa mashauri hayo.

Aidha, Tume inazikumbusha mamlaka za Nidhamu kuhakikisha kuwa Kamati za Uchunguzi zinazoundwa zinatekeleza wajibu wake ipasavyo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa taarifa zao za uchunguzi zinabainisha iwapo makosa waliyoshtakiwa nayo watumishi watuhumiwa yamethibitika au kutothibitika kutendeka. Ni muhimu pia kwa Mamlaka za Ajira kujibu barua za maombi ya ruhusa au maombi mengine ya watumishi kwa wakati ili kutowachochea watumishi hao kuvunja sheria au kuwa na malalamiko dhidi yao. Ni wajibu wa mamlaka hizo pia kuhakikisha kuwa stahiki na haki mbalimbali za watumishi zinaheshimiwa ili kupunguza malalamiko ya watumishi waliopo chini yao.

Mwisho, Tume inatoa rai kwa watumishi wote wa umma, Waajiri, Mamlaka za Ajira na na Mamlaka za Nidhamu kuendelea kufanya kazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma ili kujenga taswira nzuri ya Serikali kwa kutoa huduma bora kwa watumishi wenzetu wa umma na wananchi kwa jumla.

***KAZI IENDELEE....***

Imetolewa na:

Mathew M. Kirama

**KATIBU**

**TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

**08/03/2024**